JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM
UTUME WA FATIMA ULIMWENGUNI TANZANIA

S.L.P 79940, Dar es Salaam, Simu: 0688-946046/ 0714-000177;
Email: utumewafatimadsm@gmail.com



UTUME WA FATIMA ULIMWENGUNI.

HISTORIA YA UTUME

Kauli ya Bwana wetu Yesu Kristo Mungu kweli na Mtu kweli kuhusu Mama yake Mpendwa Bikira Maria ni hii; **“Kama kweli mnampenda Mama yangu, msikilizeni na tekelezeni maagizo yake.”** Naye Bikira Maria Mama wa Mungu anasema; **“Kwa wale wanaoshika amri za Mungu, na kuishi injili ya Bwana, ni ishara wazi kuwa kweli wanampenda Mwanangu.”** Ndiyo maana katika injili Bikira Maria anatuambia; **Lolote atakalo wambia fanyeni.**

Utume wa Fatima Ulimwenguni ni chama kinacho jikita katika kujifunza, kutekeleza na kueneza ujumbe wa Mama Bikira Maria alioutoa kule Fatima Ureno mwaka 1917. Ujumbe huu aliwapa watoto wachungaji watatu; Lusia, Fransisko na Yasinta kwaniaba ya kanisa lote.
Tukilejerea maneno ya Bwana Yesu hapo juu kwamba; **“Kama kweli mnampenda Mama yangu, msikilizeni na tekelezeni maagizo yake.”** Kujifunza, kutekeleza na kueneza ujumbe wa Fatima, ni kumwonesha Mama Bikira Maria Mapendo na hivi tunakuwa watoto wake wapenzi.

Utume wa Fatima Ulimwenguni ulianzishwa na Monsinyori Horald Colgan tarehe 24, Mei 1947 huko Amerika ya Kaskazini (USA) ukijulikana kama **Blue Army**. Kwa sasa sehemu nyingi utume huu unajulikana kama Utume wa Fatima Ulimwenguni (UFU) na hapa kwetu unajulikana kama **Utume wa Fatima Ulimwenguni Tanzania (UFUT).**

Utume wa Fatima Ulimwenguni Tanzania (UFUT) ulianzishwa na Hayati Mhashamu James D. Sangu aliyekuwa Askofu wa jimbo la Mbeya kwa wakati huo, naye ndiye alikuwa Rais wa kwanza wa UFUT baaba ya kuchaguliwa na mkutano mkuu wa kwanza uliofanyika kwanzia tarehe 16 hadi 21 Mei 1988. Kwa sasa makao makuu ya Utume wa Fatima Ulimwenguni Tanzania (UFUT) yapo jimbo kuu la Mbeya na kiongozi mkuu wa utume Tanzania ni anayekuwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Mbeya, na kwa sasa ni Askofu Mkuu Mhashamu Gervas Nyaisonga.

Mwezi Desemba mwaka huo huo wa 1988, Utume wa Fatima Ulimwenguni Tanzania (UFUT) ulizinduliwa rasmi katika jimbo kuu la Dar es Salaam na Hayati Monsinyori Deogratias Mbiku ambaye alikuwa Mkurugezi wa utume wa walei jimboni, na Paroko wa Parokia ya Chang'ombe kwa wakati huo. Uzinduzi huo ulifanyika katika parokia ya Bikira Maria wa Fatima – Msimbazi ambapo ndiyo makao makuu ya utume jimboni hadi leo. Mlezi wa utume huu ni anayekuwa Paroko wa parokia hii ya Msimbazi, na kwa sasa ni Mheshimiwa Pd. Reginald Lyimo O.F.M Cap.

UJUMBE WA FATIMA

Kama tulivyo ona katika utangulizi na historia ya utume huu kuwa madhumini yake ni kujifunza, kutekeleza na kueneza Ujumbe wa Fatima ambao upo katika vipengere vinne, lakini kwa ujumla wake ni **Toba na Mwongofu wa ndani;**

1. *Kutolea sadaka kwajili ya kufanya malipizi ya dhambi na kuwaombea wakosefu (kutakatifuza malimwengu)*
2. *Kusali Vizuri Rozari Takatifu kila siku na kutafakari matendo yake (walau mafungu matano)*
3. *Kufanya ibada ya Jumamosi ya kwanza ya mwezi kwa miezi mitano mfululizo kwa nia ya kutuliza Moyo Safi wa Mama Bikira Maria kwa makufuru yanayofanywa dhidi yake.*
4. *Kujiweka Wakfu kwa Moyo Safi wa Maria ili tuwe watoto wake wapenzi kwa kuvaa Skapulari ya kahawia ya Bikira Maria wa Mlima Karmeli kila siku*

JINSI YA KUJIUNGA NA UTUME

Ili kujiunga na Utume wa Fatima Ulimwenguni Tanzania (UFUT), mkristo mkatoliki atajifunza vizuri zaidi juu wa **Ujumbe wa Fatima** katika vipengere hivi vinne; atajifunza maana na namna ya kutolea sadaka/ kutakatifuza malimwengu, atajifunza namna zuri ya kusali Rozaria Takatifu kwa uchaji, atajifunza jinsi ya kufanya ibada ya jumamosi ya kwanza ya mwezi ambayo ni ibada ya lazima sana kwa mwongofu wa wakosefu na amani ya ulimwengu wa sasa. Ibada hii waliagiza na kuelekeza jinsi ya kufanya Bwana Yesu Kristo mwenyewe na Mama yake Mtakatifu Bikira Maria. Kwa hiyo mtakaji wa kujiunga na UFUT atalazimiza kufanya ibada hii kwa miezi mitano mfululizo kadiri ya maelekezo ya Yesu na Maria, halafu atapokelewa rasmi katika ibada ya misa Takatifu. Bahati nzuri ibada hii hufanyika kijimbo pale makao makuu ya utume parokia ya Msimbazi kila jumamosi ya kwanza ya mwezi.

Hivyo mtakaji atakuwa na nafasi nzuri ya kukutana na wanautume wengine na kujifunza zaidi. Pia mtakaji atajifunza na tutaelewa maana ya kuijiweka Wakfu kwa Moyo Safia wa Maria na maana ya Skapulari na jinsi ya kuvaa kwa ibada. Baada ya miezi hii mitano, mtakaji atapata semina maalumu ya mumwandaa kupokelewa katika utume.

Tunawakaribisha sana wakatoliki wote kujiunga na Utume wa Fatima Ulimwenguni Tanzania (UFUT) ili kuitikia wito wa Mama yetu wa Mbinguni na tuguswe na kauli ya Mwanae Yesu Kristo kwamba;
“Kama kweli mnampenda Mama yangu, msikilizeni na tekelezeni maagizo yake.”

Mama Maria …… Mama wa wote.
Tumsifu Yesu Kristo na Mama Bikira Maria.

Mawasiliano; 0714 000 177 au 0688 946 046 au 0754 283 940